ewura

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji

ISO 9001: 2015 Certified

HALIUZWI

Newsletter

JULAI 2020

ISSN 1821 - 7273 TOLEO NA. 27

Mha. Chibulunje achukua usukani

Kauli Mbiu: *"Udhibiti wa Haki kwa Matokeo CHANYA - IMPACT"*

BODI YA WAHARIRI

MWENYEKITI
Mha. Godfrey H. Chibulunje

MHARIRI
Bw. Titus M. Kaguo

MHARIRI MSAIDIZI
Bw. Wilfred Mwakalosi

WAANDISHI
Bi. Asiatu Msuya
Bi. Tobietha Makafu

MAKAO MAKUU YA EWURA,
Jengo la EWURA,
Kiwanja Na 3, Kitalu AD,
S.L.P. 2857, Dodoma,
Simu: +255 26 2329002-4,
Nukushi: +255 26 2329005,
Barua pepe: info@ewura.go.tz;
Tovuti https://www.ewura.go.tz
Simu ya BURE 0800110030

Mitandao ya Kijamii
Facebook: https://www.facebook.com/ewuranews
Twitter: https://www.twitter.com/ewuratanzania
You Tube: EWURA TV

YALIYOMO

Kutoka kwa Mhariri 3

Mhandisi Chibulunje achukua usukani 4

Tatueni malalamiko ya ankara, Mamlaka za Maji zaagizwa..... 6

Moshi, Makambako na KASHWASA mamlaka bora zaidi 7

Ewura yaendeleza vita dhidi ya vishoka..... 8

Jinsi EWURA inavyopanga bei za maji nchini..... 9

EWURA kuimarisha Elimu ya Udhibiti..... 11

EWURA ilivyotekeleza majukumu yake kipindi cha COVID-19..... 12

PICHA KUU:

Waziri wa Afy, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, Mhe. Ummy Mwalimu, akipokea mfano wa hundi ya Shilingi milioni 100 kutoka kwa Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Mha. Godfrey Chibulunje kwa ajili ya mapambano dhidi ya ugonjwa wa COVID-19, tukio lililofanyika mwezi Juni 2020 ofisini kwa Waziri Mkuu, Dodoma. Kulia ni Meneja wa Mawasiliano na Uhusiano wa EWURA, Bw. Titus Kaguo.

KUTOKA KWA MHARIRI

Wapenzi Wasomaji wetu!

Titus M. Kaguo

Wapenzi Wasomaji wetu! Ninawakaribisha wote kujiunga nasi katika toleo jipya la Jarida la Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), toleo la 27 katika mfululizo wa machapisho ya Majarida ya EWURA kwa mwaka 2020.

Kwa heshima na taadhima napenda kukualika kusoma makala za kuvutia kutoka katika shughuli mbalimbali za udhibiti zilizotekelezwa na EWURA katika kipindi cha kati ya Machi 2020 hadi Julai 2020. Toleo hili limechukua kazi za miezi mingi zaidi tofauti na utamaduni wetu wa miezi mitatu kutokana na sababu ambazo zilikuwa nje ya uwezo wetu. EWURA inadhibiti sekta ndogo tatu za nishati ambazo ni Petroli; Umeme na Gesi Asilia na Sekta moja ya Maji; Maji na Usafi wa Mazingira.

Katika kipindi hiki, EWURA imefanya maamuzi mbalimbali ya kiudhibiti ambayo baadhi yake, yamechapishwa katika toleo hili, ambalo linachapishwa katika kutekeleza maagizo ya Sheria ya EWURA Sura na 414 ya Sheria za Tanzania, kipengele cha 6(e)

Kipengele cha 6(e) kinasema kwamba ni wajibu wa Mamlaka kuhakikisha inaboresha ustawi wa jamii ya Watanzania kwa kuimarisha elimu kwa umma, ufahamu na uelewa wa sekta zinazodhibitiwa ikiwa pamoja na; haki na wajibu wa walaji na watoa huduma wa sekta zinazodhibitiwa; Njia za kutatua migogoro na kusikiliza malalamiko, kazi na shughuli za mamlaka kwa ujumla.

Katika toleo hili, pamoja na mambo mengine, habari zilizochapishwa ni pamoja na; Mhandisi Godfrey Chibulunje kuchukua mamlaka kama Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, kuendelea kwa juhudi za utoaji wa elimu kwa umma na utolewaji wa Tuzo kwa Mamlaka za Maji zinazofanya vizuri; kwa kutaja chache tu.

Karibuni!

Mhandisi Chibulunje achukua usukani

Na Mwandishi wetu

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Mha. Godfrey Chibulunje (kushoto) akipokea funguo kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Taifa la Nyumba (NHC), Dkt. Maulid Banyani kama ishara ya kumaliza shughuli za ujenzi wa jengo la EWURA lililopo Medeli Magharibi, Dodoma.

Mhandisi Godfrey Hezekiah Chibulunje ameteuliwa kuwa Kaimu Murugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA).

Mha. Chibulunje, ambaye pia ni Mkurugenzi wa idara ya Umeme, aliteuliwa tarehe 16 Aprili 2020 na Waziri wa Maji, Profesa Makame Mnyaa Mbarawa, akichukua nafasi iliyoachwa wazi na aliyekuwa akikaimu wakati huo, Bw. Nzinyangwa Mchany.

Bw. Mchany ambaye pia ni Mkurugenzi wa EWURA katika Idara ya Udhibiti wa Uchumi, aliteuliwa Januari 19, 2018, na kwamba ameitumikia nafasi hiyo kwa miaka miwili na miezi minne.

Kwa mujibu wa taarifa ya uteuzi iliyotolewa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji Profesa Kitila Mkumbo, uteuzi huo ulifanywa kwa mujibu wa sheria ya EWURA, Sura ya 414 ya sheria za Tanzania.

Profesa Mkumbo amemshukuru Bw. Mchany kwa mchango wake mkubwa kwa EWURA na kwa nchi yetu, kwa kipindi alichokuwa akikaimu nafasi ya Mkurugenzi Mkuu.

Akizungumza na uongozi baada ya uteuzi, Mhandisi Chibulunje alisema: “sifa za kuwa Mkurugenzi Mkuu EWURA ni ndogo kuliko sifa za kuwa Mkurugenzi wa Idara. Lakini kwa sababu kuna kiti kimoja tu cha Mkurugenzi Mkuu; kutakuwa na mtu mmoja tu wa kukikalia, vinginevyo wakurugenzi wote wanafaa kwenye nafasi hii.”

“Kwa kuwa serikali imeniamini mimi kukaimu nafasi hii kwa sasa,” alisema, “tafadhali tuheshimu kiti na naomba sote tushirikiane ili kuifanya EWURA iendelee kuwa bora zaidi.”
Kwa upande wake, Bw. Mchany aliwashukuru wafanyakazi wote kwa ushirikiano waliompa wakati wote alipokuwa Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa EWURA.

“Tayari nimeongea na baadhi yenu, lakini kwa wale ambao sijabahatika kukutana nao, tutaendelea kukutana kwenye shughuli zetu za kila siku,” alisisitiza.

Mhandisi Chibulunje alijiunga na EWURA mnamo mwaka 2010 kama Mhandisi Mkuu wa Umeme, akipanda hadi kuwa Meneja wa Biashara ya Umeme, na baadaye kuwa Mkurugenzi wa Idara ya Umeme, baada ya kustaafu aliyekuwa kwenye nafasi hiyo, Mhandisi Anastas Mbawala.

Mhandisi Chibulunje ana uzoefu mkubwa wa zaidi ya miaka 19 katika sekta ya nishati, hasa kwenye udhibiti. Ana uzoefu wa uongozi wa masuala ya udhibiti kwenye maeneo ya kiufundi na uchumi. Amebobea pia katika mbinu mbalimbali za kiudhibiti ikiwa ni pamoja na udhibiti wenye kuhamasisha, ushirikiano wa kikanda, udhibiti wa bei na kanuni mbalimbali za masoko ya nishati.

Tatueni malalamiko ya ankara, Mamlaka za Maji zaagizwa

Na Asiatu Msuya

Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira nchini zimetakiwa kushughulikia malalamiko yanayotokana na ankara za maji, moja ya mambo yanayolalamikiwa sana na wateja katika sekta ya maji.

Agizo hilo limetolewa hivi karibuni na Bodi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), kufuatia ongezeko kubwa la malalamiko ya ankara yaliyowasilishwa EWURA.

Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya EWURA, Bwana Ahmad Kilima, amesema aslimia 65 ya malalamiko katika sekta ya maji yanahusu bili za maji, hali inayoashiria kuwa, lipo jambo halijafanyika vizuri katika eneo hilo; hivyo kuhitaji kutizamwa kwa jicho pana zaidi ili kuhakikisha huduma inapatikana bila changamoto yoyote.

"Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya EWURA, Bwana Ahmad Kilima, amesema aslimia 65 ya malalamiko katika sekta ya maji yanahusu bili za maji, hali inayoashiria kuwa, lipo jambo halijafanyika vizuri katika eneo hilo; hivyo kuhitaji kutizamwa kwa jicho pana zaidi ili kuhakikisha huduma inapatikana bila changamoto yoyote"

"Hii inaashiria kuwa kuna Mamlaka hazitekelezi wajibu wake ipasavyo, haiwezekani malalamiko mengi yajikite katika eneo moja kwa kujirudia-rudia," alisisistiza Bw. Kilima.

Sambamba na hilo, Bodi ya EWURA imetoa rai kwa mamlaka za maji kujisahihisha katika eneo hilo, na kufanya zoezi la usomaji wa dira za maji kuwa shirikishi kati ya mtoa huduma na mteja ili kuondoa malalamiko yasiyo ya lazima.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Mhandisi Godfrey Chibulunje, akizungumzia suala hilo, amesema EWURA ina wajibu wa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwa mamlaka za maji ili kujiridhisha na utendaji wake na ufanisi wa utoaji huduma, na endapo itabainika kuwepo uzembe, hatua kali huchukuliwa.

Alisema, EWURA itaendelea na ukaguzi wake na operesheni maalum kwa mamlaka zote za maji nchini ili kujiridhisha kuhusu ankara za maji na kuhakikisha kuwa mamlaka zilizolalamikiwa katika eneo hilo, zinashughulikia malalamiko ya wateja ipasavyo.

Mamlaka za maji pia zimetakiwa kuendelea kutoa elimu kwa wateja wao kuhusu matumizi sahihi ya maji, usomaji wa dira pamoja na mabadiliko ya gharama za huduma za maji, pindi zinaporekebishwa ili kujenga uelewa, wajibu na haki za mteja katika kupata huduma.

Moshi, Makambako na KASHWASA mamlaka bora zaidi

Na Asiatu Msuya

Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira za Moshi, Makambako na KASHWASA, zimeibuka kinara kwa kushika nafasi ya kwanza katika utoaji wa huduma bora za maji na usafi wa mazingira kwa mwaka 2018/19. Mamlaka hizi pia zimefikia malengo ya kiutendaji ya utoaji huduma.

Moshi imeshinda kwa ngazi ya mamlaka za maji za mikoa, Makambako upande wa mamlaka za maji za wilaya na miji midogo; na KASHWASA, miradi ya kitaifa. Aidha, mamlaka za Iringa, Mikumi na Masasi-Nachingwea zimeshika nafasi ya pili utoaji huduma ya majisafi na usafi wa mazingira kwa ngazi ya mamlaka za maji za mikoa, wilaya na miji midogo, na miradi ya kitaifa; huku Mwanza, Biharamulo na Chalinze zikishika nafasi ya tatu.

Mamlaka nyingine zilizofanya vizuri ni Shinyanga, Maganzo na KASHWASA katika kudhibiti upotevu wa maji huku Moshi, Iringa, Dodoma, Makambako, Usa-River na Dakawa, nazo zikifanya vizuri katika uwasilishaji wa tozo ya udhibiti.

Ushindi huo umepatikana baada ya mamlaka 34 za maji za mikoa na miradi ya kitaifa na 83 za wilaya na miji midogo, kushindanishwa kiutendaji, na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), kwa kipindi cha mwaka 2018/19.

Kwa mujibu wa ripoti ya utendaji wa mamalaka za maji ya mwaka 2018/19, utoaji huduma umeimarika kwa kiwango cha maji yanayozalishwa; idadi ya watu wanaopata maji, ubora wa maji, wateja wa maji na wateja wa mtandao wa uondoaji majitaka.

Maeneo mengine yaliyoimarika ni uwiano wa wafanyakazi na idadi ya wateja, makusanyo na ufanisi wa ukusanyaji maduhuli.

Hata hivyo, ripoti hiyo pia imebainisha uwepo wa kiwango kikubwa cha upotevu wa maji, na uzalishaji mdogo ikilinganishwa na mahitaji na utoaji huduma ya uondoshaji majitaka usiokidhi mahitaji.

EWURA hufanya mapitio ya utendaji wa mamlaka za maji kwa kuzingatia Mwongozo wa Ushindanishaji na Ulinganishaji Utendaji wa Mamlaka za Maji wa EWURA wa mwaka 2018, na hutoa ripoti ya mapitio hayo kila mwaka.

Ripoti ya utendaji inayotokana na mapitio hayo ipo katika tovuti ya EWURA www.ewura.go.tz.

Ujumbe wa Bodi ya EWURA ukikagua miundombinu ya Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira ya Kahama-Shinyanga KASHWASA. KASHWASA imeibuka kuwa moja ya mamlaka bora za maji nchini kwa mwaka 2018/19.

Ewura yaendeleza vita dhidi ya vishoka

Na Tobietha Makafu



Mamlaka ya Udhibiti ya Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imeendelea na mapambano dhidi ya mafundi wanaofanya kazi za kuunganisha mifumo ya umeme bila ya kuwa na leseni za EWURA, maarufu kama vishoka.

Mtu yeyote anayefanya kifanya kazi za umeme bila leseni ya EWURA, adhabu yake ni kifungo cha miaka mitano au faini isiyozidi milioni kumi, au adhabu zote mbili kwa pamoja.

Mkurugenzi wa Idara ya Umeme katika EWURA, Mhandisi Godfrey Chibulunje amesema utoaji wa leseni za uunganishaji mifumo ya umeme unalenga kuweka utaratibu wa kisheria.

“Hatua ya kutambua mafundi umeme wenye vigezo vya kupewa leseni itaisaidia Serikali kutimiza azma ya kuhakikisha kila Mtanzania anafikiwa na umeme kwa usalama zaidi kwa kuhudumiwa na mafundi wenye vigezo,” alisema.
Mhandisi Chibulunje hatua hiyo inalenga kukabiliana na wimbi la vishoka wanaounganishia watu umeme kinyume cha sheria, hivyo kusababisha madhara makubwa kwa usalama wa watu na mali zao.”

Baadhi ya madhara yanayoweza kutokea ni pamoja na kuungua kwa nyumba, au hitilafu za mara kwa mara katika mifumo iliyounganishiwa umeme bila kufuata matakwa ya kitaaluma.

Maombi ya leseni ya umeme hufanywa mtandaoni kupitia mfumo uitwao LOIS yaani Licensing and Order Information System; unaopatikana kupitia kiunganishi https://lois.ewura.go.tz au kupitia katika tovuti ya Mamlaka www.ewura.go.tz.

Mwombaji anapaswa kuwa na nakala ya picha ya rangi ya buluu (pasipoti) wasifu (CV), vyeti vya elimu ya ufungaji umeme, risiti ya malipo ya maombi ya leseni, hati ya Kusafiria/Kitambulisho cha Taifa/Hati ya kupigia kura, na nakala za vyeti zilizothibitishwa.

Baada ya kupokea maombi, EWURA huwasiliana na chuo alichosoma mwombaji ili kuthibitisha uhalali wa vyeti alivyowasilisha. Baada ya kupata uthibitisho, maombi ya leseni huwasilishwa katika kamati ya leseni za umeme ili kupata mapendekezo ya daraja stahiki la mwombaji wa leseni.

Leseni za umeme zinatolewa katika madaraja mbalimbali kulingana na sifa za mwombaji. Daraja A ni fundi mwenye uwezo wa kufanya shughuli zote za ufungaji na usambazaji umeme, daraja B ufungaji umeme msongo wa kati hadi volti 33,000, daraja C ufungaji umeme wa msongo usiozidi Volti 400.

Mengine ni daraja D ufungaji umeme wa msongo usiozidi Volti 220, Daraja W atafanya kazi chini ya usimamizi wa mwenye leseni Daraja A, B, C au D. S1 ni daraja la kazi maalum za umeme kwa misongo yote, S2 kazi maalum za umeme wa msongo hadi Volti 33,000, S3 kazi maalum za umeme wa msongo hadi Volti 1000.

Jinsi EWURA inavyopanga bei za maji nchini

Na Tobietha Makafu

Kutathimini na kuidhinisha maombi ya bei za majisafi na majitaka nchini, ni moja ya majukumu ya kisheria yanayotekelezwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA).

Mamlaka hizi ni pamoja na mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira za Mikoa, Wilaya, Miji midogo pamoja na miradi ya kitaifa, ikiwa inatimiza jukumu lake la kudhibiti kiuchumi sekta ya Majisafi na Usafi wa Mazingira.

Utaratibu wa kupanga bei za maji nchini, huanza kwa Mamlaka ya Maji kuwasilisha maombi yake EWURA, ikiomba mabadiliko ya bei na tozo, ili kumudu gharama zilizobadilika za uendeshaji, matengenezo, umeme na kuongeza mtandao wa maji kwenye maeneo ambayo hayajafikiwa.

Katika kutathmini maombi ya marekebisho ya bei za maji, EWURA huzingatia gharama ya uzalishaji na usambazaji wa huduma, urejeshaji wa gharama za uwekezaji kwenye ujenzi wa miundombinu kama tanki hili linalojengwa na Mamalaka ya Maji Bukoba.

Katika kutathmini maombi ya marekebisho ya bei za huduma husika, EWURA huzingatia gharama ya uzalishaji na usambazaji wa huduma, urejeshaji wa gharama za uwekezaji, mlinganisho wa gharama za uendeshaji na uwekezaji na mamlaka nyingine za maji hapa nchini na nchi nyingine na pia kulinda maslahi ya wateja na pamoja na uendelevu wa huduma.

Bei za maji safi na maji taka hutolewa katika makundi ya wateja mbalimbali yakiwemo majumbani, biashara, taasisi, magati na viwanda. Tozo zinaweza kuwa ni ada ya maunganisho mapya, ada ya kurudisha huduma baada ya kusitishwa, na gharama za magari ya kusafirisha maji. Hivyo maombi hayo yanapaswa kuwa na jedwali la bei zinazoombwa lenye maelezo yanayojitosheleza, kuhusu bei zinazoombwa pamoja na mapungufu katika bei zilizopita.

Baada ya kupokea na kutathimini maombi ya marekebisho ya bei za maji kutoka mamlaka husika, EWURA hufanya uchunguzi wa kina juu maombi hayo yaliyowasilishwa, kwa kuitisha mkutano wa hadhara unaojulikana kama taftishi kabla ya kufanya maamuzi.

Kupitia taftishi EWURA inatafuta maoni ya wananchi na wadau mbalimbali wa Mamlaka ya maji katika eneo husika ili kupata maoni juu ya uhalali wa Mamlaka ya maji kuomba ongezeko hilo.

Kwa mujibu wa Sheria ya EWURA, mtu yeyote asiyeridhika na uamuzi wa EWURA anayo fursa ya kukata rufaa kwenye Baraza la Ushindani wa Haki Katika Biashara Fair Competition Tribunal (FCT).

Hivyo utaratibu wa kupitisha maombi ya kurekebisha bei za huduma za maji una hatua kuu saba ambazo ni; Kupokea maombi; Kupitia maombi na kuomba fafanuzi mbali mbali; Mkutano wa hadhara (taftishi); Kupokea maoni ya maandishi; Kufanya uchambuzi wa kina na kuwasilisha mapendekezo kwenye Bodi; Maamuzi ya Bodi; na Kutangaza maamuzi ya Bodi (Agizo) kwenye Gazeti la Serikali na katika magazeti ya kawaida.

Katika Agizo hilo, EWURA itaainisha bayana misingi, gharama na hoja zilizosababisha maamuzi yake na masharti ambayo Mamlaka ya Maji itatakiwa kuyazingatia.

Majukumu ya EWURA katika sekta ya maji yameainishwa katika Sheria ya EWURA na kutambuliwa na Sheria ya Maji ya mwaka 2019. Majukumu mengine katika sekta ya maji ni pamoja na kutoa leseni ya kutoa huduma za maji safi na usafi wa mazingira na kusimamia utekelezaji wa masharti ya leseni hiyo, kufuta leseni endapo kutakua na ukiukwaji mkubwa wa masharti yake; kudhibiti ubora na ufanisi wa utoaji huduma na kutengeneza Kanuni.

Nyingine ni kusikiliza malalamiko na kutatua migogoro katika sekta ya maji; kuelimisha umma kuhusu haki na wajibu wao katika upatikanaji wa huduma za maji nchini na kufanya kazi nyingine kwa mujibu wa sheria.

EWURA kuendelea kuimarisha elimu ya Udhibiti

Na Asiatu Msuya

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imesema itaendelea kuboresha mbinu zake za kutoa elimu ya udhibiti kwa umma ikiwemo kutumia mabaraza ya mashauriano ya mikoa na wilaya.

EWURA imechukua hatua hiyo ikitazamia kuimarisha uelewa wa wananchi na wadau wake kuhusu kazi za Mamkala, wajibu na haki za watoa huduma zinazodhibitiwa na walaji wa huduma hizo.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Mhandisi Godfrey Chibulunje, amesema hayo hivi karibuni alipokuwa akieleza vipaumbele vya Mamlaka kwa mwaka 2020.

Mhandisi Chibulunje amesema moja ya maeneo ya kipaumbele katika uongozi wake ni kuhakikisha elimu ya udhibiti inatolewa kwa ufasaha na kwa msisitizo mkubwa lengo likiwa kueleza wadau na umma kwa ujumla faida na matokea ya udhibiti unaofanywa na Mamlaka.

Kwa mujibu wa Mhandisi Chibuluje, utendaji bora wa EWURA umesifiwa hata na taasisi nyingine za udhibiti za kimataifa na imekuwa ya mfano katika kuweka mifumo mizuri ya kiudhibiti, na kwamba mafanikio haya ni lazima yaonekane kwa mwananchi wa kawaida.

“Ni wakati sasa Watanzania watembee kifua mbele na kujivunia kuwa na mamlaka kama EWURA,”alisema.

EWURA imejizatiti kuimarisha elimu kwa umma, kwa kutumia njia mbalimbali ikiwemo vyombo vya habari, mabaraza na mitandao ya kijamii kuwafikia wadau wote,

Kipengele cha 6(e) cha Sheria ya EWURA, Sura Na 414, kinaeleza kuwa Mamlaka ina wajibu wa kuhakikisha inaboresha ustawi wa jamii ya Watanzania kwa kuimarisha elimu kwa umma, ufahamu na uelewa wa sekta zinazodhibitiwa ikiwa pamoja na haki na wajibu wa walaji na watoa huduma wa sekta zinazodhibitiwa; njia za kutatua migogoro na kusikiliza malalamiko, kazi na shughuli za Mamlaka kwa ujumla.

EWURA inayo pia namba maalum ya **BURE** **0800110030** kwa ajili ya maswali na ufafanuzi wa masuala mbalimbali ya kiudhibiti. Simu ya mkononi inaweza kutumika pia kufahamu bei ya mafuta kwa kupiga ***152*00#** na kufuata maelekezo.

EWURA ilivyotekeleza majukumu yake kipindi cha COVID-19

Na Asiatu Msuya

Siku za hivi karibuni, Tanzania, kama zilivyo nchi nyingine, ilipata mlipuko wa ugonjwa unaosababishwa na virusi vya corona (COVID-19). Hali hii ilisababisha Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), kama zilivyofanya taasisi nyingine, kuchukua hatua mbali mbali kama tahadhari za kudhibiti kuenea kwa maambukizi ya virusi hivyo.

Baadhi ya hatua hizo ni kubadili mwelekeo wa uendeshaji wa shughuli za kiudhibiti, ikiwemo kujikita zaidi kutoa elimu kwa njia ya redio, televisheni, tovuti na mitandao ya kijamii na kuepuka kuendesha kampeni za uhamasishaji na elimu kwa umma na mikutano yote ya hadhara inayovutia mikusanyiko mikubwa.

Pili ni, kuendesha taftishi ya marekebisho bei za huduma kwa kutangaza magazetini, kupokea maoni kupitia mitandao ya kijamii, barua pepe, masanduku ya maoni na kuzuia mikutano ya ana kwa ana na wadau.

Hatua nyingine ni kuhimiza matumizi ya mitandao ya kijamii na njia nyingine za kieletroniki kupata huduma zinazotolewa na Mamlaka kama kuomba leseni, vibali vya ujenzi na kuwasilisha malalamiko ya huduma zinazodhibitiwa.

Aidha, EWURA imehimiza pia kwa watumishi wake kuendesha mikutano kwa tahadhari kubwa, na iwapo ni lazima, kushiriki kwa makundi ya watu wachache, kukaa umbali wa angalau mita mbili, kuvaa barakoa na kutakasa mikono kila wakati ili kuendelea kujikinga na maambukizi ya COVID-19.

Ingawa hatua hizi zimeonesha kubadili utamaduni uliozoeleka katika utekelezaji wa baadhi ya majukumu ya Mamlaka, utekelezaji wa majukumu hayo umekuwa wenye ufanisi maukbwa.

Hata hivyo, yapo majukumu ambayo utekelezaji wake umeathirika kwa kiasi fulani. Mamlaka inaendelea kutafakari zaidi, namna bora ya kuhakikisha watoa huduma zinazodhibitiwa wanatekeleza wajibu wao kwa kufuata masharti ya leseni, usalama, afya na mazingira katika utoaji wa huduma.

EWURA inaendelea kusimamia sekta na kuhakikisha kuwa huduma za kutosha za majisafi na salama zinaendelea kupatikana ili kurahisisha vita dhidi ya COVID-19 pamoja na kuendelea kuimarisha ushiriki wa wadau, utoaji wa elimu ya udhibiti kwa umma.



> "Mamlaka inaendelea kutafakari zaidi, namna bora ya kuhakikisha watoa huduma zinazodhibitiwa wanatekeleza wajibu wao kwa kufuata masharti ya leseni, usalama, afya na mazingira katika utoaji wa huduma."